## UTANGULIZI

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini, ambayo inalenga kuimarisha nguvukazi iliyo katika soko la ajira kiujuzi.

## HALI HALISI YA SOKO LA AJIRA

Utafiti wa Nguvu Kazi wa mwaka 2014 unaonesha kuwa, takriban asilimia 79.9 ya nguvukazi ya Taifa ina kiwango cha chini cha ujuzi; asilimia 16.6 ya nguvukazi ina kiwango cha kati cha ujuzi; na asilimia 3.6 ya nguvu kazi ina kiwango cha juu cha ujuzi. Kiwango cha ujuzi kinachokubalika kuwezesha nchi za uchumi wa kipato cha kati ni angalau asilimia 12 kwa kiwango cha juu cha ujuzi, asilimia 34 kwa ujuzi wa kiwango cha kati na chini ya asilimia 54 kwa ujuzi wa kiwango cha chini.

### CHIMBUKO LA PROGRAMU YA KUKUZA UJUZI

Programu hii ilitokana na changamoto iliyoibuliwa na waajiri kwamba mara nyingi wameshindwa kuwaajiri wahitimu kwa sababu hawana ujuzi wa kuweza kuwaajiri ingawa wengi wao wana shahada. Kamati ya kusimamia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini inayosimamia eneo la Sheria za Kazi na Ukuzaji Ujuzi ilikubaliana kuandaa Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini ambayo ilianza kutekelezwa mwaka 2015, ikiwa na lengo la kukuza ujuzi wa nguvu kazi nchini.

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU


Programu hii imewalenga vijana wa kike, wakiume, watu wenye ulemavu na watu waliopo katika Soko la Ajira kwa maana ya walioajiriwa na watafuta kazi, ili kuwawezesha kupata ujuzi unaotakiwa katika soko la ajira.
Programu hii inatekelezwa kwa kutumia njia zifuatazo:-

### (a) Mafunzo ya Uanagenzi (Apprenticeship training)


Mafunzo ya ufundi ambayo mhusika hutumia asilimia 40 ya muda wake kwa masomo ya nadharia darasani na asilimia 60 ya muda wake kwa masomo ya vitendo sehemu ya kazi. Katika utekelezaji wa mafunzo, programu hii imegawanyika katika sekta mbalimbali za kipaumbele ambazo ni: Mafuta na Gesi; Ujenzi; Usafiri na Usafirishaji; Utalii na Ukarimu; TEHAMA na Viwanda. Mafunzo haya yanaratibiwa na Mwongozo wa Kitaifa wa Mafunzo ya Uanagenzi (National Apprenticeship Guidelines).

#### (i) Ufundi

Mafunzo haya huchukua muda mfupi, wa kati na mrefu kulingana na aina ya ujuzi na hutolewa kwa watu wa ngazi mbalimbali za elimu.



Tangu kuanza kwa mafuzo haya jumla ya **vijana 17,191** wamepatiwa mafunzo katika fani za ushonaji nguo, useremala, uashi, terazo, uchorongaji wa vipuri, ufundi magari, ufundi umeme, ufundi bomba, uchomeleaji na uungaji vyuma, mapishi na usindikaji wa vyakula, utengenezaji wa samani kwa kutumia "aluminium" na uchapaji wa nyaraka, ufundi wa viatu vya ngozi na TEHAMA na **vijana 5,875** wanaendelea na mafunzo.



#### (ii) Kilimo cha kisasa


Kwa kutumia mfumo wa mafunzo kwa vitendo na nadharia, Serikali inatoa mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa teknolojia ya kitalu nyumba katika Halmashauri 84 za Mikoa ya Lindi, Ruvuma, Dodoma, Manyara, Mwanza, Simiyu, Kagera, Shinyanga, Geita, Iringa, Mbeya na Kilimanjaro.
Jumla ya Vitalu Nyumba 87 vimejengwa katika Halimashauri husika. Aidha, vijana 8,700 wamepa mafunzo ya kilimo hicho pamoja na kujenga vitalu nyumba. Lengo ni kufikisha ujuzi huu kwa vijana 18,800 katika Halmashauri zote za Tanzania Bara.



Serikali pia imegharamia vijana 100 kuhudhuria mafunzo ya kilimo cha kisasa nchini Israeli.

### (b) Kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo

Mafunzo haya yanahusisha kutambua watu wenye ujuzi uliopatikana katika mfumo wa mafunzo usio rasmi, kuwapa mafunzo ili kuziba mapungufu yatakayobainika na kuwapatia vyeti. Kwa kutumia vyeti hivyo wanaweza kujiendeleza kielimu, kuboresha huduma wanazotoa na kutafuta ajira au kujiajiri.



Tangu kuanza mafunzo haya jumla ya **vijana 14,432** wamepewa mafunzo na kurasimishwa ujuzi na kupatiwa vyeti katika fani za Uashi, Useramala, Ufundi magari, Upishi na Huduma za hoteli.

### (c) Mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi kwa Wahitimu (Internship training)

Mafunzo haya yanahusisha vijana waliohitimu ngazi mbalimbali za elimu ambapo watapatiwa fursa ya kujifunza kwa vitendo katika maeneo ya kazi. Muda wa mafunzo haya ni miezi sita hadi mwaka mmoja. Mafunzo haya huwapatia vijana uzoefu wa kazi na kuwawezesha kuajiriwa au kujiajiri. Wahitimu 1,287 wamewezeshwa kupata mafunzo ya vitendo mahala pa kazi katika fani mbalimbali. Aidha, vijana 890 wamepata ajira kutokana na uzoefu walioupata katika mafunzo.

### (d) Mafunzo ya kukuza ujuzi kwa walio makazini

Mafunzo haya yanalenga kujenga uwezo wa nguvukazi iliyopo kazini ili iendane na mabadiliko ya teknolojia na kufanya kazi kwa weledi zaidi ili kuongeza tija na ufanisi kazini na pia kuongeza uwezo wa ushindani wa nchi katika soko la ajira.

0715803900

## SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2019 HADI 2020


Kipindi cha mwaka 2019 hadi 2020 Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini imepanga kutoa mafunzo yafuatayo:

i. Kutoa mafunzo ya ukuzaji ujuzi kwa njia ya uanagenzi kwa **10,000;**
ii. Kurasimisha Ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi kwa vijana **10,000;**
iii. Kutoa mafunzo kwa vitendo mahali pakazi kwa Wahitimu **5000;**
iv. Kutoa mafunzo ya kilimo cha kisasa na kuongeza thamani ya mazao kwa vijana **20,300;**
v. Kutoa mafunzo kwa vijana **2,000** walio katika sekta isiyorasmi juu ya kurasimisha biasharana ujasiriamali.

Tunawasihi vijana kuendelea kufuatilia na kuomba nafasi tunapotangaza fursa hizi.

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**

# PROGRAMU YA KUKUZA UJUZI NCHINI



Imeandaliwa na
Idara ya Ajira na Ukuzaji Ujuzi